Department of Education
GOVERNMENT OF WESTERN AUSTRALIA

# Njia za kwenda Chuo Kikuu

## Taarifa kwa wazazi na walezi

Wanafunzi wa shule za madarasa ya juu wanaweza kuchagua kutoka katika njia mbalimbali za kwenda chuo kikuu, mafunzo na ajira. Njia zinaweza kuchaguliwa ili kukidhi maslahi ya wanafunzi, ujuzi, mahitaji na matarajio.

## Ni njia gani za kwenda chuo kikuu?

### ATAR

Kiwango cha Wanafunzi Waliokubaliwa kwenda Elimu ya Juu ya Australia (ATAR) hukokotolewa kwa kutumia kozi yao na matokeo ya mitihani. Angalau kozi nne za ATAR zinahitajika. Kwa wanafunzi wengi, asili ya kitaaluma na changamoto ya kozi za ATAR hutoa maandalizi bora ya kufaulu chuo kikuu.

Ili kuweza kuchaguliwa kwenda chuo kikuu kama mwanafunzi wa shule kwa kutumia ATAR, wanafunzi lazima:

- kukidhi mahitaji ya Cheti cha Elimu cha Australia Magharibi
- kufikia kiwango cha Umahiri wa Lugha ya Kiingereza kama ilivyobainishwa na kila chuo kikuu, kupitia mojawapo ya:
  - ATAR Kiingereza
  - ATAR Kusoma
  - ATAR EAL/D au sawa (alama iliyopimwa ya 50 au zaidi)
  - mahitaji ya chini kabisa katika Jaribio Maalum la Kuandikishwa kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (STAT) kwa Kiingereza.
- kupata ATAR ya juu ya kutosha kwa ajili ya kuingia kwenye kozi fulani, na
- kukidhi sharti lolote au mahitaji maalum ya kuingia kwenye kozi fulani.

Wanafunzi wa mwaka wa 12 wanapewa taarifa kuhusu kutuma maombi kwenda vyuo vikuu na kuandikishwa kwa kozi za shahada ya kwanza na shule zao.

### ATAR iliyo na Marekebisho ya Kiwango cha Uteuzi

Baadhi ya wanafunzi wanastahiki marekebisho ya ATAR. Marekebisho huongeza nafasi ya mwanafunzi kutokana na mambo kama vile:

- ufaulu katika masomo ya Mwaka wa 12
- kuishi au kuhudhuria shule katika eneo fulani
- kuwa wa kwanza katika familia kuhudhuria chuo kikuu, au
- kustahiki kwenye Miradi ya Kuata Elimu.

Mwanafunzi anaweza kuwa na nafasi tofauti za uteuzi kwa vyuo vikuu tofauti. Kwa taarifa zaidi, tembelea:

| Chuo kikuu | Tovuti |
|---|---|
| **Curtin** | https://study.curtin.edu.au/applying/pathways/stepup-to-curtin |

D22/0035704
9/02/2022
CC BY Exclusions may apply

| | |
|---|---|
| **Edith Cowan** | https://www.ecu.edu.au/__data/assets/pdf_file/0011/676946/ECU-Access-Eligible-WA-Schools.pdf |
| **Murdoch** | https://www-uat.murdoch.edu.au/study/pathways-to-uni/high-school/selection-rank-adjustment |
| **Chuo Kikuu cha WA** | https://www.uwa.edu.au/study/how-to-apply/admission-entry-pathways/broadway |

## Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET)

Wanafunzi wanaweza kutumia sifa za VET ili kukidhi mahitaji ya chini zaidi ya kuingia katika kozi mbalimbali za shahada ya kwanza. Kawaida waombaji wamefanikiwa kupata WACE, wamekamilisha sifa katika kiwango cha Cheti cha IV na kukidhi Uwezo wa Lugha ya Kiingereza. Kwa taarifa zaidi, tembelea:

| Chuo kikuu | Tovuti |
|---|---|
| **Curtin** | https://study.curtin.edu.au/applying/pathways/tafe-vet |
| **Edith Cowan** | https://www.ecu.edu.au/future-students/course-entry<br>Wanafunzi wanaweza kutumia Cheti cha III na ujuzi wa lugha ya Kiingereza kuomba kuingia katika kozi za ECU UniPrep, kwa Taarifa Zaidi tembelea.<br>https://www.ecu.edu.au/degrees/uniprep |
| **Murdoch** | https://www-uat.murdoch.edu.au/study/pathways-to-uni/vocational-education-and-training<br>Wanafunzi wanaweza kutumia Cheti cha II katika Elimu ya Jumla kwa Watu Wazima au Cheti III na ujuzi wa lugha ya Kiingereza ili kutuma maombi ya kujiunga na programu za OnTrack na FlexiTrack za Murdoch. Kwa taarifa, nenda kwa:<br>• OnTrack - https://www-uat.murdoch.edu.au/course/enabling/n1069<br>• FlexiTrack - https://www-uat.murdoch.edu.au/course/enabling/n1095 |
| **Chuo Kikuu cha Notre Dame** | https://www.notredame.edu.au/study/pathways/vet-study<br>Inapatikana kwa kozi nyingi isipokuwa Sheria, Utaalamu wa Viungo (Physiotherapy) na Elimu. |
| **Chuo Kikuu cha WA** | https://www.uwa.edu.au/study/How-to-apply/Admission-entry-pathways/Diploma-Entry-Pathway |

## Njia za Wanafunzi wa asili ya Australia na wa Torres Strait Islander

Kuna njia maalum kwa wanafunzi wa asili ya Australia na wa Torres Strait Islander kuingia chuo kikuu. Kwa taarifa zaidi, tembelea:

| Chuo Kikuu | Tovuti |
|---|---|
| **Curtin** | https://karda.curtin.edu.au/study/enabling-courses |


D22/0035704
9/02/2022
Exclusions may apply

| | |
|---|---|
| **Edith Cowan** | Tathmini ya Utayari wa Chuo Kikuu kwa wananchi wa asili ya Australia (AURA) inaruhusu wanafunzi ambao wamemaliza Cheti cha II au cha chini kuzingatiwa ili kuingia chuo kikuu. Kwa taarifa, nenda kwenye https://www.ecu.edu.au/centres/kurongkurl-katitjin/student-success-and-support/aborignal-university-readiness-assessment |
| **Murdoch** | Mpango wa kuwezesha K-Track ni kozi ya bila malipo inayowawezesha wananchi wa asili ya Australia na Torres Strait Islanders kuanza na elimu ya juu au kutafuta mabadiliko katika mwelekeo. Kwa taarifa, nenda kwenye https://www.murdoch.edu.au/life-at-murdoch/perth-campus/facilities-services/kulbardi-aboriginal-centre/k-track-enabling-program |
| **Chuo Kikuu cha Notre Dame** | Notre Dame wana fursa kadhaa na njia mbadala za kuingia kwa wanafunzi wa wananchi wa asili ya Australia na wa Torres Strait Islander kusomea Udaktari. Kwa taarifa, nenda kwenye https://www.notredame.edu.au/current-students/support/indigenous-portal |
| **Chuo Kikuu cha WA** | Fursa za masomo kwa wazawa: Chuo Kikuu cha Australia ya Magharibi kinajumuisha kozi ya Mwelekeo wa wananchi wa asili ya Australia na mpango wa Kuingia kwa Muda. Kwa tarifa, nenda kwenye https://www.uwa.edu.au/study/indigenous-study |

### Kozi za Maandalizi ya Chuo Kikuu

Maandalizi ya chuo kikuu au kozi za kuwezesha zimeundwa ili kuwatayarisha wanafunzi kufuzu katika kozi mbalimbali za shahada ya kwanza. Kozi hizi zinazingatia ujuzi unaohitajika kwa masomo ya ngazi ya chuo kikuu kama vile utafiti, michakato ya kuandika na kuhesabu. Kwa taarifa zaidi, tembelea:

| Chuo Kikuu | Tovuti |
|---|---|
| **Curtin** | Mpango wa UniReady haulipishwi na uko wazi kwa wanaomaliza shule na wanafunzi waliokomaa. Kwa taarifa, nenda kwenye https://study.curtin.edu.au/applying/pathways/uniready-enabling-program |
| **Edith Cowan** | Kozi za UniPrep ni za bure na ziko wazi kwa wanaomaliza shule na wanafunzi waliokomaa. Kwa taarifa, nenda kwenye https://www.ecu.edu.au/degrees/uniprep |
| **Murdoch** | Murdoch ina njia mbalimbali zinazowezesha. Kwa taarifa, nenda kwenye http://www.murdoch.edu.au/study/courses/enabling-pathways |
| **Chuo Kikuu cha Notre Dame** | https://www.notredame.edu.au/study/pathways/tertiary-pathway-program |

### Kuingia kwa kuzingati mafanikio

Wanafunzi wanaweza kuchukuliwa kuingia katika kozi maalum za shahada ya kwanza kupitia njia nyingine inayoonyesha mafanikio ya kitaaluma, sifa, uwezo, na kufaa kwa


D22/0035704
9/02/2022
Exclusions may apply

masomo ya juu. Kwa taarifa zaidi, tembelea:

| Chuo kikuu | Tovuti |
| --- | --- |
| **Curtin** | Kuingia kwa kuzingatia mafanikio kunapatikana kwa kozi mbalimba za ubinadamu, sayansi, biashara na sayansi ya afya. Kwa taarifa, nenda kwenye https://study.curtin.edu.au/applying/pathways/portfolio-entry |
| **Edith Cowan** | Wanafunzi wanaweza kuchukuliwa kuingia kwenye kozi maalum za shahada ya kwanza katika taaluma za sanaa ya ubunifu na usanifu bila ATAR. Kwa taarifa, nenda kwenyehttps://www.ecu.edu.au/future-students/course-entry/creative-arts-portfolio-entry |
| **Murdoch** | Njia ya vyombo vya habari ni ya wanafunzi wabunifu wanaolenga kujiandikisha katika kozi ya Sanaa. Kwa taarifa, nenda kwenye:<br>• https://www.murdoch.edu.au/study/courses/undergraduate-courses/portfolio-entry-pathway<br>• http://www.murdoch.edu.au/study/courses/undergraduate-courses/portfolio-entry-pathway/media-portfolio-pathway |

## Kuingizwa kulingana na uzoefu

Wanafunzi wanaweza kuchukuliwa kuingia kozi ya shahada ya kwanza kupitia tathmini ya chuo kikuu ya uwezo wao wa kufaulu katika elimu ya juu kulingana na ushahidi uliotolewa. Kwa taarifa zaidi, tembelea:

| Chuo kikuu | Tovuti |
| --- | --- |
| **Curtin** | Inaweza kuwasaidia wanafunzi kupata nafasi ya kujiunga na kozi wanayopendelea ikiwa hakuna njia nyingine inayofaa. Kwa taarifa, nenda kwenye https://study.curtin.edu.au/applying/pathways/access-curtin |
| **Edith Cowan** | Huwaruhusu wanafunzi kupewa nafasi ili kuingia kwenye kozi ya shahada ya kwanza kupitia tathmini ya uwezo wao wa kufaulu katika elimu ya juu. Kwa taarifa,nenda kwenye https://www.ecu.edu.au/future-students/course-entry/experience-based-entry-scheme |
| **Chuo kikuu cha WA** | Hutoa chaguo lililotathminiwa au lisilotathminiwa ili kusoma vitengo vyao binafsi bila hitaji la kujiandikisha katika kozi ya shahada. Kwa taarifa nenda kwenye https://www.uwa.edu.au/study/courses-and-careers/short-courses/access-uwa-assessed |

## Mpango wa Ufikiaji wa Elimu

Wanafunzi ambao wamekumbana na hali za kipekee wakati wa shule ya juu, ambayo imeathiri vibaya masomo yao ya Mwaka wa shule wa 11 na 12, wanaweza kutafuta uandikishaji wa shahada ya kwanza katika vyuo vikuu vya Australia Magharibi. Waombaji wanaweza kutuma maombi ya kuzingatiwa kiekee kupitia Kituo cha Huduma ya Taasisi zaaa Juu (TISC).

Kwa taarifa zaidi, tembelea tovuti ya TISC www.tisc.edu.au/static/guide/eas.tisc


D22/0035704
9/02/2022
cc BY Exclusions may apply